

# EKKLESIA

## BARAZA LA WATAKATIFU

PASTOR JAMES KALEKWA

# EKKLESIA:

*Baraza la Watakatifu!*

James Kalekwa

# Yaliyomo Barazani:

Salamu za Mama Mchungaji JK. 4

Tangazo kuhusu Ekklesia .......... 6

Muundo wa neno Ekklesia.......... 9

Ekklesia hupatikana wapi?........ 11

Ekklesia ni Takatifu .................. 15

Tumeitwa kutoka wapi? (Tofauti ya wajumbe wa Ekklesia na watu wengineo)................................ 20

Tumeitwa kuelekea wapi?......... 26

Madhihirisho ya Utakatifu kwa wana-Ekklesia.......................... 34

Kuhusu New Vine Church:....... 44

Mawasiliano na Mwandishi: ..... 45

# Salamu za Mama Mchungaji JK.

Juni 20, Mungu alitupa zawadi ya maisha ya mtumishi wake Pastor JK, mtu wa juhudi nyingi katika Kristo na maarifa ya kimungu. Kwa muda ambao nimekuwa naye kwenye maisha, nimemtambua kama mtu anayempenda Mungu kiasi cha mimi kukosa neno la kuelezea. Huyu ni mtu aliuzwa kwa Mungu na utumishi!

Amewekeza muda mwingi kuandika mfululizo wa vitabu hivi vya kielektroniki ili avitoe bila malipo kama sehemu yake ya ujenzi wa mwili wa Kristo… kwa niaba yake, ninaomba ukipokee kwa kuthamini dhabihu! Ninakuombea ya kwamba maisha yako yanageuzwa kwa kitabu hiki kimoja tu kwa jina la Yesu Kristo.

Pili, ninaomba uwasambazie kitabu hiki watu wengi zaidi ili maono ya kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari yatimilizwe.

Na hatimaye, kwa kuthamini zawadi ya mtu huyu wa Mungu, muombee, mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumsherehekea ukimweleza namna gani umesadika na utumishi wake – itafaa sana.

Heri ya siku ya kuzaliwa mume wangu mpenzi. Heri ya kuzaliwa Pastor JK – zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu!

Frida James Kalekwa (Mama mchungaji JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2025
Dodoma, Tanzania

# Tangazo kuhusu Ekklesia

Mathayo 16:18SUV *"Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu* ***nitalijenga kanisa langu****; wala milango ya kuzimu haitalishinda."*

Kwa mara ya kwanza neno kanisa linapotokeza kwenye Maandiko Matakatifu ni mahali hapa na utaona mahali pa kijiografia alipokuwa Bwana Yesu na jambo analolizungumza vina uhusiano mkubwa!

Kijiografia, kwenye andiko hili Bwana Yesu alikuwa eneo liitwalo Kaisaria-Filipi (rejea Mathayo 16:13). Kwenye machapisho ya kihistoria, inaonekana kuwa

eneo hili la Kasaira-Filipi lilifahamika kama *"lango la kuzimuni"*. Kulikuwa na mwamba mkubwa ambao chini yake kulikuwa na mapango. Huko ndiko iliaminika ya kuwa miungu ya mji hupitia kutokea kuzimuni. Chini ya bonde, mapangoni, kwa sababu rutuba palivutia kufanyika ibada humo ya mungu aitwaye *"Pani"- Nusu mtu, nusu mnyama (mbuzi)!* Kwenye Agano la Kale mji huu ulifahamika kama Baal-hermoni au Baal-gadi.

Nataka ung'amue hili ya kwamba Bwana Yesu Kristo anatoa tangazo la kuzaliwa kwa kanisa akiwa amesimama juu ya mwamba ambao chini yake ndimo kuna malango ya kuzimu. Kisha anasema, "...

*wala malango ya kuzimu haitalishinda (kanisa)”*. Kama aliposimama ni eneo kutisha, ni malango ya kuzimu na Yesu anazungumza kuwa yuko mbioni kufanya mageuzi kwa kuinua kanisa. Hili dude linaitwa kanisa linapaswa kuwa ni dude kubwa na la kustaajanisha sana kiwango ambacho kuzimu haiwezi mudu nguvu yake.

## Muundo wa neno Ekklesia

Neno “Kanisa” kama linavyoonekana kwenye Agano Jipya au kama alivyolitumia Bwana Yesu wakati akitoa tangazo, linatokea kwenye lugha ya Kiyunani (Kigiriki) “Ekklesia” – ambao ni muunganiko wa maneno mawili: i). ek na ii). kaleo

Ek-kutoka kwa…

Kaleo lina maana ya kuita au kualika

Hivyo basi neno *Ekklesia* lina maana ya walioitwa/walioalikwa kutoka kwa.., kuwatenga kutoka eneo la jumla. Maana ya kuitwa ni jambo la jumla lakini kuitikia ni

jambo binafsi na wale walioitikia ndio huunda kusanyiko/baraza la Ekklesia.

2 Wakorintho 6:17SUV *"Kwa hiyo, Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha."*

Dhana ya tokeni kati yao ina maana ya kuwepo na tofauti kati ya wengine na wewe mtakatifu (Kanisa). Yaani hao wanaorejelewa kama “kati yao” ni watu wengineo; na huyo anayeambiwa “Tokeni” ni mtu tofauti na hao ijapokuwa ametoka kwao na ametokana na wao!

## Ekklesia hupatikana wapi?

Ekklesia (walioitwa) inaelezea mambo haya;

1. Kanisa la ulimwengu

Waefeso 1:22SUV *"akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa"*

Moja ya kweli tunapaswa kujua ni hii, kanisa la ulimwengu wote (universal Church) halitawahi kuja kukaa pamoja wala kuonana hapa duniani. Hii ni jumla ya waliookoka wakati uliopita, uliopo na ujao. Ni jumla ya wanaoliitia jina la Bwana sehemu mbalimbali ulimwenguni.

2. Kanisa la Mahala pamoja

1 Wakorintho 1:2SUV *"kwa kanisa la Mungu* ***lililoko Korintho****, wale waliotakaswa katika Kristo Yesu, walioitwa wawe watakatifu, pamoja na wote wanaoliitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo kila mahali, Bwana wao na wetu."*

Ufunuo 1:11SUV *"ikisema, Haya uyaonayo uyaandike katika chuo, ukayapeleke kwa hayo makanisa saba:* ***Efeso, na Smirna, na Pergamo, na Thiatira, na Sardi, na Filadelfia, na Laodikia****."*

Hili ni kanisa linalokusanyika pamoja kwenye eneo la kijiografia kama

yalivyotajwa kwenye rejea za Maandiko hapo juu.

3. Waamini waliokusanyika pamoja kwa ajili ya ibada.

Mt 18:20 (SUV), *"Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao."*

Hii ni aina ya kusanyiko ambalo si kanisa la mahala pamoja, bali limekuja pamoja kwa ajili ya ibada kwa muda fulani husika. Mathali semina, warsha, makongamano na mambo ya namna hiyo. Mungu huwaona kuwa ni kanisa!

4. Waamini walioko eneo au ukanda wa kijiografia.

Matendo 9:31SUV *"Basi kanisa likapata raha katika* ***Uyahudi wote na Galilaya na Samaria****, likajengwa, likiendelea na kuongezeka katika kicho cha Bwana, na faraja ya Roho Mtakatifu."*

Biblia inawatambua na kuwaona wamini walio kwenye ukanda mmoja wa kijiografia, ingawa huwa hawakutani pamoja kama kanisa la mahala pamoja, kuwa ni kanisa. Waamini wa mkoa kata, wilaya, mkoa, nchi fulani… Hutambuliwa kama kanisa la eneo hilo linalotajwa.

## Ekklesia ni Takatifu

Mara zote utaona kuna jambo Mungu anapambana na kila aliyeinuka dhidi ya Watakatifu wake waliopo duniani na hao anawatambua kuwa wao ni "Kanisa" na kila aliyewagusa watu hao Mungu aliitikia kwa kusema ameguswa Yeye mwenyewe. Na hii ni kwa sababu Yeye ndiye mmiliki wa kanisa hivyo kuwagusa watakatifu wake ni kumgusa yeye moja kwa moja.

Matendo 9:4-5NENO *"Akaanguka chini, akasikia sauti ikimwambia, "Sauli, Sauli, mbona unanitesa?"5Sauli akajibu, "U nani wewe, Bwana?"*

Ile sauti ikajibu, "***Mimi ni Yesu unayemtesa***." Kumgusa Mtakatifu wa

Bwana ni kumgusa Bwana Yesu moja kwa moja, hivyo kwako mwamini huu uwe ni ujasiri wako kuhusiana na mambo mbalimbali uyaendee kutokea kwenye ufahamu huu kuwa kuhusiana na jambo lolote linakupokea kama Mtakatifu wa Bwana Yesu na si pungufu ya hapo.

Mtume Paulo analitambulisha kanisa la watu wa Korintho kuwa pamoja na mambo madhaifu yanayoendelea kwenye maisha kama sehemu yao ya ukuaji kimwenendo (Soma kitabu kiitwacho KADOSH utaona nimefafanua madara mawili ya Utakatifu: 1. Kinafasi 2. Kimwenendo) yao ni kwamba Bwana amewaita hapo wawe watakatifu.

1 Wakorintho 1:2SUV *"kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho, wale waliotakaswa katika Kristo Yesu,* ***walioitwa wawe watakatifu,*** *pamoja na wote wanaoliitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo kila mahali, Bwana wao na wetu."*

2 Wakorintho 1:1SUV *"Paulo, mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu, na Timotheo ndugu yetu; kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho,* ***pamoja na watakatifu wote*** *walioko katika nchi yote ya Akaya."*

Mara zote nyaraka kuyaelekea makanisa yote katika Biblia imeyatambulisha na watu wake kuwa ni **watakatifu** bila ya kujali hali na matendo waliyokuwa wakiyafanya kwa wakati huo! Ni jambo zito sana hili

kukubaliana nalo kwa mara moja. Kwenye kitabu cha Zaburi isemwapo kweli ambayo inataka "Upigane mieleka" kukubaliana nayo, hutumika neno "Selah!" yaani, tulia utafakari.

Hivyo tunafikia kwenye hitimisho ya kwamba nafasi ya utakatifu wa ekklesia na wajumbe wake ni kusudio la Mungu. Kwa hiyo hili ni baraza la watakatifu kwa nafasi tu ya kuitwa humo na kwa sababu hiyo wanatakiwa kuanza "*kupambana*" kuwa watakatifu kimwenendo sawasawa na ujumbe wao kwenye baraza! Mwamini anapaswa kutambua kuwa ni wajibu wake kuenenda kwenye utakatifu.

Neno linatambua kuwa ni jambo la kawaida na inapaswa kuwa hivyo, yaani mwamini aenende na alinganie utakatifu alioukusudia Bwana Yesu kwa sababu ameitwa kuwa hivyo!

Ekklesia ni jumuisho la *walioitwa*, *kutoka*, *waliotengwa*, *kuwekwa kando*, *waliotofautishwa*… zote hizo ni dhana za neno Ekklesia.

## Tumeitwa kutoka wapi? (Tofauti ya wajumbe wa Ekklesia na watu wengineo)

Kuitwa maana yake ni kutenganishwa kutoka kwenye kundi kubwa “*be summoned”*.

Kila wito unaambata na kubadilishwa yale yaliyokuwa utambulisho wa awali. Ekklesia ni kuitwa kutoka kwenye mambo ambayo yalikuwa ni stahiki kulingana na upande uliokuwa unamilikiwa. Mwamini ameitwa kutoka kwenye mambo haya yafuatayo;

I. *Mautini*

Waefeso 2:1,5, *“1.Nanyi* ***mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu****; 5. hata wakati ule* ***tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu;*** *alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema.”*

Ni mtiririko wa asili alikokua mwanadamu kabla ya kupokea neema ya wokovu ambayo ililetwa na Bwana Yesu ya kwamba mwanadamu alikua ni mfu, yaani hana uhai ndani yake na hivyo alikua hafai kwa lolote lile. Sababu ya umauiti ndani ya mwanadamu ni makosa na dhambi! Kwa sababu hiyo basi, mtu yeyeote aliye katika hali ya makosa na dhambi yumo mautini hali anaishi.

Ekklesia ni wito wa kutoka kwenye hali ya umauti; ni kutengwa mbali na mauti na kuwa kwenye uzima wa milele.

Yohana 17:3SUV “Na ***uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe,*** Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma”

Uzima wa milele kwa tafsiri ni kumjua Yeye, Mungu wa pekee na kweli, na Yesu Kristo aliyemtuma. Ukiulizwa swali kwenye mtihani, “Uzima wa milele ni nini?” majibu ndiyo hayo.

Wajumbe wote wa Ekklesia, si kwamba wanajivuna, bali ujumbe wao kwenye baraza hili huja nahadhi ya kutoka mautini. Wengine wote wako mautini!

II. *Gizani*

1 Petro 2:9SUV "Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita ***mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu***;"

Giza ni mahali mwanadamu aliishi, mambo yote aliyaona kutokea kwenye ufahamu huo na hakukua na namna ya kutoka huko isipokuwa uhusika wa neema ya Mungu kuingilia kati, Hivyo Ekklesia ni kuitwa kutoka gizani! Wengine wote wamo gizani na wanaenenda gizani isipokuwa tu wajumbe wa Ekklesia.

Isaya 60:2, *“Maana, tazama, **giza litaifunika dunia, Na giza kuu litazifunika kabila za watu**; **Bali BWANA atakuzukia wewe**, Na utukufu wake utaonekana juu yako.”*

Yohana 3:19, *“Na hii ndiyo hukumu; ya kuwa nuru imekuja ulimwenguni, **na watu wakapenda giza kuliko nuru;** kwa maana matendo yao yalikuwa maovu.”*

Unaona huo ulinganifu baina ya makundi mawili? Kuna kundi linarejelewa na Maandiko kama kundi la dunia, kabila za watu, au watu. Kisha kuna kundi ambalo linatajwa kimahususi kabisa kuwa ni wewe! Hilo ndilo kundi la Ekklesia na wajumbe

wake. Ni watu ambao nuru imewazukia (imekuja ulimwenguni).

III. *Dhambi*

2 Timotheo 1:9SUV *“ambaye alituokoa* ***akatuita kwa mwito mtakatifu****, si kwa kadiri ya matendo yetu sisi, bali kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema yake.”*

*1 Wathesalonike 4:7SUV "Maana Mungu hakutuitia uchafu,* ***bali tuwe katika utakaso****."*

Mwamini amepokea wokovu kwa njia ya wito mtakatifu kutoka kwa Bwana Yesu,

kutengwa mbali na dhambi imetokana na uhusika wa kuitwa na Yesu.

## Tumeitwa kuelekea wapi?

Mara zote hakuna kuitwa bila ya kuelekezwa wapi pa kuelekea! Uelekeo ndiyo unaelezea maana ya kuitwa, hivyo maana ya kuitwa imebebwa na uelekeo ni wapi! Kukosa uelekeo inapoteza maana ya kuitwa, hivyo Ekklesia ni kuitwa na kuna uelekeo kuuhusu huo wito. Ekklesia ni kuitwa kuelekea wapi? Tupate majibu ya swali hili.

*i. Kuelekea ufalme wa Mungu*

Jambo la muhimu kwa mwamini anapaswa kutambua kuwa yeye si raia wa eneo lolote lile tofauti na kitu kinafahamika kama ufalme wa mbinguni na/au ufalme wa Mungu. Hivyo utambulisho wake ni kwamba yeye ni wa mbinguni na si pungufu ya hapo.

Wakolosai 1:13-14SUV "Naye alituokoa katika nguvu za giza, ***akatuhamisha na kutuingiza*** katika ufalme wa Mwana wa pendo lake; ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi;"

Mwamini anapaswa kutambua kuwa amehamishwa kihadhi kuwa raia wa ufalme mwingine. Kwa sababu hiyo, anapaswa kuwa na mwenendo unaofanania hadhi

yake mpya ya uraia – ujumbe wake wa Ekklesia!

Dunia kote hatuna raia wa ufalme wa mbinguni isipokuwa tu wajumbe wa Ekklesia.

*ii. Kuwa wa moja pamoja na kristo*

1 Wakorintho 1:9SUV *"Mungu ni mwaminifu ambaye mliitwa na yeye mwingie katika ushirika wa Mwanawe, Yesu Kristo Bwana wetu."*

Mwamini amekusudiwa kuwa pamoja na kwa umoja na Bwana Yesu wakati wote kwenye kila jambo na sio kwenye mambo kadhaa. Kila jambo limekusudiwa kuendewa na mwamini kutokea kwenye

uhakika ya kwamba yeye ni mwana wa Mungu. Na mrithi pamoja na Kristo Yesu.

*iii. Kwenye ushirika wa imani pamoja na waamini wengine, yaani kuwa mwili mmoja.*

Wakolosai 3:15SUV "***Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu;*** ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja; tena iweni watu wa shukrani."

Waefeso 2:19, *"Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji,* ***bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu.****"*

Wenye kanisa ninalochunga, nimefundisha kwa nguvu na kwa kurudia-rudia sana ya

kwamba sisi si kanisa la mjini bali ni kanisa la kibiblia… Sasa, kibiblia Ekklesia ni kuwa ndugu… kuwa familia… kuwa wenyeji kwenye "kaya" ya Mungu.

Hivyo basi, ni sawa kutambua ya kwamba kama mjumbe wa baraza la watakatifu umeitwa ili upewe ndugu wa kike na wa kiume. Tena hawa siyo ndugu ambao unaweza kuwa na mashaka na vinasaba… hawa ni ndugu katika damu. Damu bora zaidi, yaani damu ya Yesu Kristo.

Luka 10:29-30, *"Yesu akasema, Amin, nawaambieni, Hakuna mtu aliyeacha nyumba, au ndugu waume, au ndugu wake, au mama, au baba, au watoto, au mashamba, kwa ajili yangu, na kwa ajili ya*

*Injili, 30ila atapewa mara mia sasa wakati huu, nyumba,* ***na ndugu waume, na ndugu wake, na mama, na watoto,*** *na mashamba, pamoja na udhia; na katika ulimwengu ujao uzima wa milele."*

Mwamini tambua kuwa unaweza kujiunga kwenye mambo mengi yanayohusu shughuli mbalimbali na za muhimu tu, lakini linapokuja swala la kanisa tambua hakuna awezaye kujiunga na kanisa kwa sababu kujiunga ni jambo la kimaamuzi na hivyo kuna nafasi ya kuamua kutoka pia. Hivyo katika muktadha wa kanisa mwamini huwa anakua mwanafamilia, yaani kanisa linampokea na anaishi namna linavyotaka jenyewe na hapa ndipo linakuja swala la

nini kanisa linataka na limepangiliwa hivyo ndivyo na mwamini atakavyokuwa hakika. Kuelewa kwa mapana fundisho kuhusu kanisa, tafadhali soma kitabu kiitwacho ***“Kanisa la mahala pamoja”*** nilichokitoa mwaka 2024.

*iv. Kushiriki mwito wa mbinguni*

Waebrania 3:1SUV *"Kwa hiyo, ndugu watakatifu,* ***wenye kuushiriki mwito wa mbinguni****, mtafakarini sana Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, Yesu,"*

Mwamini amekusudiwa kuitika mwito wa Kristo Yesu na kwa maana hiyo namna ya kuyaendea mambo iamuliwe na mwito huu kwa Bwana wake.

*v. Kuelekea utakatifu*

Waebrania 3:1SUV "*Kwa hiyo, ndugu watakatifu, wenye kuushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, Yesu,"*

Mungu anatarajia kwamba ni lazima iwepo tofauti inayoonekana kati ya wanaofika kwenye baraza lake (Ekklesia) na ambao hawapaswi kufika. Kama mhusika wa baraza hili yaani mwana Ekklesia kuna namna unatarajiwa kuonekana na hata namna unavyotenda kazi inapaswa iwepo tofauti kati ya mwana Ekklesia na watu wa aina nyingine yoyote ile.

## Madhihirisho ya Utakatifu kwa wana-Ekklesia.

Wakolosai 3:1-2SUV, "Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. ***Yafikirini yaliyo juu***, siyo yaliyo katika nchi."

*Basi ikiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo!* Hii sentensi inafikirisha sana.. ni kama vile mwandishi hana uhakika na "sisi" aliotuandikia. Anaweka *mzigo wa lawama* kwetu. Kama kweli tumefufuka pamoja na Kristo; kama tunajinasibu ya kuwa

tumeokoka na ni wajumbe wa Ekklesia kuna viwango tunatarajiwa kuonekana navyo.

Namna ya mwanadamu anavyoenenda inaamua na inazungumza kwa sauti kuwa ni mambo gani unayoyafikiri na inasema kwa sauti kuhusu yeye ikiwa amefufuliwa au hajafufufliwa pamoja kristo.

Hivyo tunapata kwa uwazi kuwa mwamini anapaswa kutajwa kwenye kuyatafuta ***yaliyo ya juu*** na si chini ya hapo pia namna yake ya kufikiri ni kuyaelekea yaliyo ya juu tu kinyume cha hapo kuna ujumbe unatumwa kuwa huyu hafai na hawezi kuwa mwana Ekklesia. Au inawezekana ya kwamba hajafufuka pamoja na Kristo.

Mtume Paulo anatambulisha madhihirisho ya utakatifu na katika maeneo mbalimbali na anasema kila usdhihirisho una athari kwenye eneo husika na kuna matokeo yanaambatana na udhihirisho husika. Kila udhihirisho wa utakatifu umefungamanishwa na vitu fulani ambavyo na viko tofauti na udhirisho mwingine kabisa: Mfano katika udhihirisho wa utakatifu kibinafsi, kifamilia na hata kikazi za mikono na madhihirisho mengine yote hayo kuna namna mtakatifu amekusudiwa aonyeshe utakatifu kote huko kama mwana Ekklesia.

a) Madhihirisho kibinafsi (Wakolosai 3:5-11)

Kuna neno kali sana hapa anatumia Mtume kuelezea wajumbe wa Ekklesia kwenye madhihirisho binafsi ya utakatifu. “Vifisheni…” (Mstari 5)… ni sawa na kusema ueni, chinjeni… maliza kabisa! Mjumbe wa Ekklesia ni *“katili kiasi hicho”* linapokuja swala la yeye na mwenendo wa utakatifu. Usisahau sentensi ilikotokea, “…mkiwa mmefufuliwa…” Kama kweli wewe ni mjumbe wa Ekklesia, hivi ndivyo viwango vyako.

Kisha anaendelea mbele kufafanusha mambo kadhaa ya utakatifu kibinafsi. Mjumbe ashughulike nayo yeye mwenyewe huko sirini. Nimedokeza tu ili upate muda wa kutafiti mwenyewe kwa msaada wa Roho wa Mungu kupitia Maandiko Matakatifu.

Mungu akinipa neema nitaandika kitabu kinachohusu "Sura za Mwenendo" kwenye mafundisho ya neema ya Mtume Paulo.

b) Madhihirisho katika ushirika (Wakolosai 3:12-17) – Hapa mtume anaonyesha ya kwamba baada ya kumalizana na nafsi yake, mjumbe

wa Ekklesia anapaswa kudhihirisha utakatifu katika mahusiano na watu wengine. Kuna maagizo kwenye Biblia huitwa maagizo ya kutendeana au maagizo ya ninyi kwa ninyi. Haya yametolewa kwa waamini tu. Jukwaa lake la utekelezaji ni kwenye kanisa la mahala pamoja hasa.

Unaona maneno kama mkifundishana na kuonyana? Kwa ujumla wake, tazama sentensi zinazotumika hapo ni za upamoja si za mtu mmoja!

Kama kweli umefufuliwa pamoja na Kristo hivyo ndivyo unavyotarajiwa kuwa.

c) Madhihirisho katika ndoa na familia (Wakolosai 3:18-21)

Haya ni maelekezo ya uendeshaji wa ndoa na familia za waamini tu… ni kwa ajili ya wajumbe wa Ekklesia. Ukitumia Maandiko haya kuwafundishia wasio wajumbe wa Ekklesia, ni kama unawaonea. Ni kama kuongoza taifa la

Sudani Kusini kwa kutumia katika ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ndiyo maana maelekezo kwenda kwa wake wana Ekklesia na kisha waume wana Ekklesia kisha wazazi wana Ekklesia na watoto wao. Hayo ni magumu na kama vile hayawezekani kwa wasio watakatifu. Kimsingi, kufanya hivyo ndiyo kudhihirisha utakatifu. Hii ndiyo inapaswa kuwa mstari unaopambanua ndoa za wana Ekklesia na za watu wengineo wasio wajumbe kwenye baraza hili muhimu!

Haya yanawezekana kama tu umefufuka pamoja na Kristo… kama huwezi,

unapaswa kuwa na mashaka na ujumbe wako barazani. Inawezekana wewe si mjumbe lakini unadhani tu ya kuwa u mjumbe.

d) Madhihirisho katika kazi za mikono (Wakolosai 3:22-25) – Kwenye kipengele hiki, mtume anashughulika na wana Ekklesia wawapo kwenye kazi zao za mikono. Wakiwa kama watumwa/waajiriwa; ama wakiwa kama mabwana/waajiri.

Umeona ni kwa namna gani Ekklesia na wajumbe wake wanatarajiwa kuwa?

**Kuhusu Mwandishi:**

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor, Priscilla na Butogwa; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

**Mawasiliano na Mwandishi:**

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: Pastor James Kalekwa

Instagram: @pastorjameskalekwa

Youtube: Pastor James Kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

NEW VINE CHURCH | Dodoma



New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

**Ratiba za Ibada**

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni
**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma  +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor ,Priscilla na Butogwa. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa
+255 754 917 764
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
MchungajiJK
+255 754 917 764
jameskalekwa.com